



# SHIRIKA LA TIJA LA TAIFA

## KOZI YA KUJIANDAA NA MAISHA YA BAADA YA KUSTAAFU KAZI

### Malengo ya Kozi

Lengo kuu la mafunzo haya ni kuwapa washiriki mbinu za kisasa zitakazowawezesha kujiandaa vyema na maisha baada ya kustaafu ajira rasmi. Mafunzo haya pia ni fursa mahsusi kabisa kwa washiriki kupata uzoefu wa mambo mbalimbali baada ya kustaafu.

### Walengwa

Wote walio kwenye ajira rasmi.

### Mada Muhimu

Wakati wa mafunzo washiriki watapata nafasi ya kujifunza yafuatayo: Kufikiria kuhusu kustaafu; Maisha baada ya kustaafu; Jinsi ya kupanga kustaafu; Uwekezaji na Bima; Mpango wa biashara; Kilimo na ufugaji; Pensheni; Huduma za kibenki; Uwekezaji; Kuandaa mpango wa utekelezaji; Usimamizi wa fedha; Afya ya wafanyakazi; Mazoezi ya uzeeni, Mafunzo kwa vitendo (field visit).

### Matarajio

Baada ya mafunzo haya washiriki wataweza kupata mbinu mbalimbali za kujiandaa vizuri zaidi na maisha ya baada ya kustaafu ajira rasmi.

### Mbinu za Mafunzo

Mchanganyiko wa Mafunzo na mazoezi kwa vitendo, mazoezi kwa vikundi, Uwasilishaji wa mada mbali mbali.

### Lugha ya Mafunzo

Kiswahili

### Mahali

Morogoro – Kituo cha Tushikamane

### Muda

Wiki moja

Kundi Na	TAREHE	
	Kuanza	Kumaliza
Moja	19 Agosti, 2019	23 Agosti, 2019
Mbili	7 Oktoba, 2019	11 Oktoba, 2019
Tatu	02 Desemba, 2019	06 Desemba, 2019
Nne	10 Februari, 2020	14 Februari, 2020
Tano	20 Aprili, 2020	24 Aprili, 2020
Sita	01 Juni, 2020	05 Juni, 2020

### Ada na Utaratibu wa Malipo

Ada ni Tshs. 715,000/= na inatakiwa ilipwe kabla ya kuanza kozi kupitia akaunti ya Shirika la Tija la Taifa kwenye Benki ya CRDB, Namba ya Akaunti 01J1042999200, Tawi la Tower; kinyume na hapo mshiriki hataruhusiwa kuhudhuria kozi.

### Jambo la Kuzingatia

Tafadhali zingatia kuwa gharama za safari, chakula na malazi zitagharamiwa na taasisi itakayokudhamini kwenye kozi. Ada yetu imejumuishia gharama za ufundishaji, gharama za utawala, viburudisho vilaini wakati wa asubuhi. Unatakiwa utoe taarifa kwenye ofisi zetu za NIP hapa Dar es Salaam kabla ya kuripoti kwenye mahali pa mafunzo.

### Wasiliana nasi

Nyumba ya Maarifa, Mtaa wa Ohio  
S.L.P 2021, Dar es Salaam, Tanzania,  
Simu: (+255) 22 2110523/ 2126832/ 2126981 and (+255) 769 291905  
Nukushi: (+255) 22 2128619/ 2126081  
Barua pepe: [info@niptz.org](mailto:info@niptz.org)  
Tovuti: [www.niptz.org](http://www.niptz.org)